Haliuzwi
SEPTEMBA 30, 2025
/islamicftz
Rabi' II 8 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 552
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Forest Hill yatajwa fahari ya Moro UK 7



# Ulimwengu wamlilia Mufti Mkuu wa Saudi Arabia



(1943–2025)

إنا لله وإنا إليه راجعون

Sheikh Dkt. Saleh bin Humaid, Mufti Mkuu mpya na Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wanazuoni.



## Mkakati wa Bandari ya Dar kushughulikia ongezeko la mizigo

UK 10

## Trump awa mbogo UN

■ Wakati Rais Donald Trump akisema kutambua taifa la Palestina ni "zawadi kwa Hamas," viongozi wengine, akiwamo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, wameunga mkono kuanzishwa kwa taifa huru la Palestina.

UK 14



HABARI KIMATAIFA

UKHTI FATIMA SS




Mufti Mkuu wa Saudi Arabia, Sheikh Abdulaziz al-Sheikh enzi ya uhai wake, akiongoza swala katika msikiti wa Imam Turki bin Abdullah mjini Riyadh, Saudi Arabia

# Ulimwengu wamlilia Mkuu wa Saudi Arabia

Innā lillāhi wa innā ilayhi rājiūn. Ulimwengu wa Kiislamu umemuaga msomi na kiongozi mnyenyekevu aliyejitolea maisha yake katika kazi ya kulingania, kufundisha dini na kutetea na kufafanua mafundisho ya Uislamu.

Sheikh Abdulaziz bin Abdullah Al-Sheikh, Mufti Mkuu wa Ufalme wa Saudia na Mkuu wa Baraza la Wanazuoni Wakuu, aliaga dunia Jumanne, Septemba 23, 2025, akiwa na umri wa miaka 82. Taarifa ya Ikulu ya Kifalme ilieleza kwa huzuni kwamba Umma wa Kiislamu umepoteza msomi aliyetoa mchango mkubwa katika ibada, maadili na ujenzi wa jamii.

Kwa zaidi ya miaka ishirini, alikuwa nguzo ya ushauri wa kisheria na dira ya kijamii, akiongoza taasisi za dini kwa utulivu na uadilifu. Sauti yake ilisikika kwa upole na uthabiti, ikiwaletea waumini matumaini, maelekezo ya dalili na hamasa ya kuishi kwa uchaji Mungu katika nyakati zote.

## Maisha, elimu na urithi wa kielimu

Sheikh Al-Sheikh alizaliwa Makka mwaka 1943, ndani ya ukoo wa Al Āl-Sheikh, urithi unaounganisha kizazi cha wanazuoni na historia ya kujenga misingi ya dini na maadili katika jamii ya Kiislamu. Tangu utotoni, alijitolea kuhifadhi Qur'an na kusoma fiqhi, hadith na misingi ya aqida, akilea ndani yake upendo wa elimu, unyenyekevu na bidii isiyochoka.

Baada ya kuhitimu Kitivo cha Sharia katika Chuo Kikuu cha Imam Muhammad ibn Saud mwaka 1963, alifundisha katika taasisi za dini na baadaye kuwa mhadhiri katika Taasisi ya Juu ya Mahakama (Higher Institute of Judiciary) jijini Riyadh. Safari hii ya ualimu ilimpa jukwaa la kuandaa maelfu ya wanafunzi, kuwalea katika staha, uthibitisho wa dalili na kuheshimu tofauti za kifiqhi ndani ya mipaka ya Sharia.

Kuteuliwa na uongozi kama Mufti Mkuu

Mwaka 1996, aliteuliwa Naibu Mufti Mkuu, hatua iliyomwandaa kwa jukumu kubwa zaidi la kitaifa. Mwaka 1999, kufuatia kufariki kwa Sheikh Abdulaziz bin Baz, akateuliwa kuwa Mufti Mkuu wa Ufalme wa Saudia, nafasi aliyoishikilia hadi umauti ulipomkuta.

Kupitia wadhifa huu, aliongoza Baraza la Wanazuoni Wakuu na Kamati ya Kudumu ya Utafiti wa Kiislamu na Utoaji wa Fatwa, akiratibu kazi za utafiti, ushauri na utoaji wa fatwa zilizoongoza ibada na maisha ya kila siku ya waumini.

Katika kipindi chake cha uongozi, alisimamia utoaji wa maelekezo ya kisheria yenye kuleta wepesi wa utekelezaji wa dini katika mazingira yanayobadilika, huku akidumisha utiifu wa misingi ya Qur'an na Sunna. Uwepo wake katika taasisi za juu za dini uliimarisha uaminifu wa jamii kwa taasisi hizo, na kufanya maamuzi ya kifiqhi yawe taa ya kuongoza waumini ndani na nje ya Saudia.

Khutba ya Hija na majukwaa ya ibada

Sheikh Al-Sheikh alitambulika sana kama khatib wa Msikiti wa Namira, Arafat, ambako alitoa khutba ya Hijja kila mwaka kwa takriban miaka 35. Hotuba zake ziliwapatia mahujaji mwanga wa Tauhidi, wito wa toba na kusisitiza umoja, rehema na haki—mafunzo yanayoakisi roho ya Hijja na kusafisha mioyo ya Waumini wanaokusanyika kutoka pembe zote za dunia.

Katika misimu ya Hijja na Umra, nasaha zake zilitumainisha mamilioni ya mahujaji. Kupitia maneno yenye busara na rejea thabiti za dalili, aliwasaidia Waumini kurudi makwao wakiwa na azma mpya ya kutenda mema, kuimarisha familia zao na kuchangia amani na maadili mema katika jamii.

## Huduma kwa Sharia na maendeleo ya kijamii

Kama mfasiri rasmi wa Sharia ya Ufalme, alitoa fatwa na mwongozo wa kisheria katika masuala yanayogusa ibada, familia, uchumi na maslahi mapana ya jamii. Uongozi wake uliweka urari kati ya kuhifadhi turathi za elimu ya Kiislamu na kujibu maswali ya zama, hivyo kufanya mafundisho yawe yaeleweke na kutekelezeka na watu wa rika na mazingira tofauti.

Katika kipindi cha mageuzi ya kijamii nchini, alisaidia kutoa mwongozo unaoleta wepesi wa utekelezaji wa sheria za dini kwenye huduma za umma, elimu, na maisha ya kijamii. Msururu wa maelekezo yake ulisaidia kuimarisha nidhamu, heshima kwa sheria na utulivu wa jamii, huku ukiheshimu misingi ya haki, huruma na ustawi wa watu.

UKHTI FATIMA SS

# SHEIKH DKT. SALEH AL-HUMAID



## Mufti Mkuu mpya Saudi Arabia

Ufalme wa Saudi Arabia umemteua Sheikh Dkt. Saleh bin Abdullāh Al-Humaid kuwa Mufti Mkuu wa Saudi Arabia na Mwenyekiti wa Baraza la Wanazuoni Wakuu, akiichukua nafasi iliyoachwa wazi na marehemu Sheikh Abdulaziz bin Abdullah Al-Sheikh.

Taarifa za vyombo kadhaa vya habari vya kikanda na kimataifa zinasema kuwa uteuzi huu unaashiria kipindi kipya katika uongozi wa taasisi za dini nchini humo, ukizingatia hadhi yake kama Imam na Khatibu wa Masjid al-Haram kwa zaidi ya miongo minne na msomi wa juu wa fiqhi.

Kwa mujibu wa ripoti hizo, mchakato wa uteuzi ulitokea siku chache tu baada ya kutangazwa rasmi na Saudi Press Agency (SPA) kufariki kwa Mufti Mkuu wa zamani siku ya Jumanne, Septemba 23, 2025.

### Wasifu na hadhi ya kielimu

Sheikh Dkt. Al-Humaid ni mmoja wa wasomi wanaoheshimiwa zaidi katika ulimwengu wa Kiislamu. Amehudumu kama Imam na Khatib wa Masjid al-Haram kwa zaidi ya miongo minne, na mara kwa mara hutumikia pia kama mhadhiri na msomi wa fiqhi wa ngazi ya kimataifa.

Nafasi yake katika taasisi za kimataifa ni pamoja na Rais wa Baraza la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (IIFA) yenye makao yake Jeddah, chombo cha kitaaluma cha Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) kinachojishughulisha na tafiti za juu za fiqhi/usharia na kutoa mwongozo wa kisheria wa Kiislamu kwa masuala ya kisasa ya kijamii, kiuchumi, kielimu na kitamaduni. Makao makuu yako Jeddah, Saudi Arabia.

Miongoni mwa heshima alizopokea ni Tuzo ya Kimataifa ya Mfalme Faisal – Huduma kwa Uislamu (2016), ikithibitisha mchango wake wa kielimu na kijamii katika kufafanua fiqhi ya masuala ya wakati. Tovuti ya tuzo hiyo inanukuu safari yake ya masomo na majukumu ya juu serikalini kama mshauri wa Ikulu ya Kifalme na kiongozi wa taasisi za elimu ya juu za Kiislamu.

### Elimu, taaluma na uongozi wa taasisi

Kihistoria, Al-Humaid alikulia katika nyanja za elimu ya Kiislamu, akihitimisha shahada ya kwanza, ya uzamili (Masters) na uzamivu (PhD) katika Fiqh na Usūl al-Fiqh - Umm al-Qura/Makkah. Aidha, amekuwa mwanachama wa Majlis al-Shura (Baraza la Ushauri) tangu 1993, na aliwahi kuwa Spika/Mwenyekiti wa baraza hilo katika miaka ya 2000, jambo lililompa mtazamo mpana wa kiutawala unaounganisha ujuzi wa fiqhi na sera za umma.

Kwenye uwanja wa Hijja, Al-Humaid anafahamika ndani na nje ya Saudi Arabia kwa kuongoza au kutoa khutba ya Arafa (Namira) katika nyakati mbalimbali, jukumu linaloonesha heshima na imani ya taifa kwa sauti yake ya kiibada. Taarifa za mwaka 2025 pia zilithibitisha kuteuliwa kwake kutoa khutba ya Arafa, kupitia tangazo la taasisi ya masuala ya kidini ya Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Mtume.

### Majukumu mapya kama Mufti Mkuu

Kama Mufti Mkuu, Al-Humaid ataongoza Baraza la Wanazuoni Wakuu na Kamati ya Kudumu ya Utafiti wa Kiislamu na Utoaji Fatwa, na kutoa maoni ya kisheria (fatwa) kuhusu masuala ya ibada, familia, uchumi na maisha mapana ya kijamii.

Vyombo vya habari vya kikanda vimebainisha kuwa uteuzi wa kiongozi mwenye mizizi imara katika Haramain na pia uzoefu wa bunge la ushauri unaleta mchanganyiko wa uongozi wa kiroho na uwezo wa kiutawala, jambo linalotarajiwa kuimarisha mawasiliano kati ya taasisi za dini, serikali na jamii.

### Sifa bainifu: uandishi na mchango wa fiqhi

Mbali na uongozi wa ibada, Dkt. Al-Humaid ameandika na kusimamia tafiti nyingi za fiqhi zinazoangazia familia, fiqhi za majanga ya wakati (nawāzil), adabu za majadiliano, na kuondoa mashaka katika utekelezaji wa Sharia kwenye masuala mapya.

Wasifu wa IIFA na vyanzo vingine vinamrejea kama msimamizi wa jitihada za ijtihād za pamoja (collective ijtihad) ndani ya jumuiya za fiqhi za kimataifa.

المؤسسة الإسلامية
The Islamic Foundation

# CHANGIA GAZA




**Mixx by Yas: 0716 542 323**
Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION

**M-Pesa: 0768 111 877**
Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION

**CRDB Bank: 0150657264700**
Account: THE ISLAMIC FOUNDATION

**Lipa kwa simu: 15441517**
Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION

**Airtel Money: 0696 568 625**
Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION

NA UKHT FATMA S

# Wahitimu sekondari na chaguo gumu la kwenda chuo au kidato cha 6

Wakati tunaelekea mwishoni mwa mwaka, ni wakati pia ambapo familia zenye vijana wanaohitimu kidato cha nne na darasa la saba watakabiliwa na jukumu gumu na kubwa litakaloamua mustakabali wa watoto wao.

Jambo lenyewe ni: je, baada ya Kidato cha nne, kijana aende kidato cha tano au chuo cha kati? Uamuzi wa pili mgumu ni anaenda kusomea nini—yaani mchepuo gani kwa aendaye Kidato cha Tano, na fani gani kwa aendaye chuo cha kati—lakini pia aende chuo au shule gani.

Chuo cha kati au kidato cha tano?

Kuna faida na hasara kwa kila chaguo kati ya hayo mawili. Kwa wanaoenda chuo moja kwa moja, huenda kusomea fani zinazoweza kuwapa ujuzi mahsusi—kama unesi, ukunga, ufundi mitambo, uongozaji watalii, usimamizi wa hoteli, uandishi wa habari na kadhalika—na hivyo kupata fursa ya kuajiriwa au kujiajiri mapema tu, mara tu wamalizapo masomo yao.

Kwa upande wa sekondari ya juu—kidato cha tano na sita—ni ngazi nzuri ya kupanua ufahamu wa mwanafunzi kwa kuongeza elimu ya nadharia, badala ya fani mahsusi ya kutenda kazi kama ilivyo kwa vyuo vya kati.

Kwa maana nyingine, kiuhalisia, mtu aliyesoma kidato cha tano na sita anakuwa amepanua uelewa wa mambo na hivyo kuandaliwa vyema kwa elimu ya chuo kikuu, hasa kwa wanaoenda kusoma programu za taaluma za kinadharia zaidi kama sayansi ya siasa, uchumi, saikolojia n.k. Tatizo linabaki kuwa akimaliza haajiriki katika fani mahsusi hadi afike chuo kikuu na kupata ujuzi katika fani fulani.

Kuna suala la muda ambako tunaona tofauti nyingine. Wakati kumaliza kidato cha sita kunahitaji miaka miwili, kule chuoni aghalabu programu nyingine ni miaka mitatu au hata zaidi. Hata ukizingatia unahitimu chuo ukiwa na ujuzi mahsusi, pengine mwaka mmoja zaidi si tatizo. Baadhi ya watu huona muundo wa usomaji katika vyuo vya kati kuwa rahisi kwa sababu ya mgawanyo wa vipindi viitwavyo semesta, ambapo kila semesta (wiki 15–20) ina masomo na mtihani wake. Kwa maana nyingine, ukimaliza semesta na kufanya mtihani, unahamia masomo mengine yenye mitihani yake isiyokuhitaji kukumbuka masomo yote ya semesta zilizopita ili ufaulu.

Kwa upande wa kidato cha tano hadi sita, hatima ya mwanafunzi huamuliwa katika mitihani ya mwisho ya kuhitimu ngazi hiyo. Haijalishi uwezo ulioonesha njiani; kama hukuwa vizuri katika kipindi cha mitihani na ukafeli, ina maana hatima yako imeamuliwa. Hivyo, mwanafunzi anahitaji nidhamu kubwa ya kujisomea kila mada aliyosoma kwa miaka miwili ili afaulu mitihani—kazi ngumu kwa wanafunzi wasiopenda kujisomea.

Kwa upande mwingine, katika mfumo wa vyuo kuna kazi za darasani zinazochangia maksi kwenye mitihani (kuanzia 40–60 kati ya 100), na hata mwanafunzi akifeli, ana nafasi ya pili katika mwaka huo huo wa masomo kurekebisha kwa kufanya upya somo alilofeli.

Kwa wale wahitimu wa Kidato cha nne walioamua kusoma hadi Kidato cha Sita, wajue: licha ya hatima yao kuamuliwa kwenye mtihani wa mwisho, iwapo watafeli hawana njia nyingine zaidi ya kusubiri kufanya mtihani upya mwakani—jambo linalopoteza muda.

Uzoefu unaonesha wapo waliofaulu Kidato cha nne na kupata maksi za kwenda chuo cha kati, lakini walipoenda sekondari ya juu mwishowe walifeli na kurejea kutumia maksi za Kidato cha nne kwenda tena chuo cha kati—hivyo kama kupoteza muda.

Ukiacha faida na hasara za kila chaguo, mambo mengi yazingatiwe katika kufanya uamuzi. Ni muhimu mzazi atambue utashi wa mwanafunzi—anataka nini; na ajue uwezo wake wa kitaaluma, kwani ni wazi kidato cha tano na sita kunahitaji nguvu kubwa ya kusoma.

Wapo wanafunzi ambao tayari wanajua wanataka kusomea nini na wana haraka ya kuingia kwenye fani husika. Hawa—ikiwemo wanaotaka uuguzi, ukunga, ufundi mitambo, ufundi umeme, ukatibu mahsusi—vyuo vya kati vinawafaa zaidi.

Mtoto anayewaza kuwa profesa kama Lipumba kwenye uchumi au Baregu kwenye siasa, bila shaka njia ya kidato cha sita inaweza kumfaa zaidi kuliko kwenda vyuo vya kati; sawa pia na wasomi wa sayansi za lugha, fasihi na kadhalika.

Hali ya kipato cha familia pia izingatiwe. Kwa mtoto anayetoka familia yenye kipato kidogo, chuo cha kati kinaweza kuwa bora zaidi kwa sababu atapata sifa ya kuajirika au kujiajiri mapema; hata kama uwezo wa kumpeleka chuo kikuu utakosekana, atakuwa na cha kufanya.

Zamani ilidhaniwa wenye ufaulu mdogo ndio huenda vyuo vya kati kusomea fani kama ualimu n.k., lakini siku hizi ufaulu si kigezo pekee. Wapo wengi wenye daraja la kwanza Kidato cha nne waliowahi kuamua kwa makusudi kwenda chuo, aghalabu kusomea kozi ngumu kama tiba, uhasibu na uhandisi.

## Suala la maadili

Kuna tofauti kubwa za mtindo wa maisha vyuo vya kati ukilinganisha na sekondari ya juu. Vyuoni, wanafunzi wana uhuru mkubwa zaidi kwa sababu vyuo vingi havijihusishi sana na udhibiti wa kinidhamu katika mambo yaliyo nje ya taaluma. Ni muhimu mzazi kujua hili ili ajue namna ya kumchunga mwanawe bila kutegemea walimu, tofauti na shule.

Kama chuo kiko mbali na nyumbani, mwanafunzi anaweza kukaa hosteli, lakini baadhi yao huharibikiwa kimaadili kutokana na uhuru uliopitiliza. Mzazi, kuzuia hilo, anapaswa kuweka mfumo wa uangalizi kwa namna moja au nyingine.

Pengine njia nzuri ya kudhibiti maadili ya mwanafunzi ni kumpeleka katika vyuo vya taasisi za dini ambavyo, licha ya kufundisha taaluma husika, pia hufundisha masomo ya dini na kusisitiza maadili. Kwa bahati nzuri, vyuo hivyo vikipewa nguvu na Waislamu kwa kupelekewa watoto wao vitaimarika zaidi.

## Shule gani au chuo gani?

Tumeona kuwa kigezo muhimu cha uchaguzi wa shule au chuo ni maadili, lakini kiwango cha ufaulu na taaluma pia ni muhimu—ikiwemo kwa Darasa la Saba wanaoenda Kidato cha Kwanza.

Uamuzi wa kumpeleka mtoto shule ya bweni au kutwa ni muhimu, na kila chaguo lina faida na hasara. Mtoto anapokaa nyumbani, mzazi anapata fursa ya kumfuatilia na kujua maendeleo yake katika nyanja zote za maisha, na kujenga mahusiano ya karibu.

Wapo watoto ambao, kutokana na kukaa bwenini maisha yao yote ya masomo, ukaribu na wazazi umekuwa mdogo na hivyo kukosa mtu wa karibu wa kuwangoza. Hata hivyo, wapo watoto ambao kukaa bwenini ni bora kwa ajili ya udhibiti kwa sababu wanapenda michezo mingi. Vilevile, kwa wanafunzi wenye maradhi makubwa ni bora kukaa nyumbani au kusoma shule ya bweni iliyo karibu na makazi ya mzazi.

ربيع ثان

**HABARI MOROGORO**

NA MWANDISHI WETU



# Forest Hill yatajwa fahari ya Morogoro

Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro umeipongeza Shule ya Sekondari ya Forest Hill, inayomilikiwa na Taasisi ya The Islamic Foundation, kwa si tu kufaulisha wanafunzi kwa asilimia mia moja bali pia kusimamia maadili.

Afisa Elimu Manispaa ya Morogoro (Sekondari), Deogratius Mhaiki, amesema ufaulu wa Forest Hill umechangia kwa kiasi kikubwa kukuza viwango vya ufaulu vya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ukilinganisha na halmashauri nyingine kimkoa na kitaifa.

Mhaiki alitoa kauli hiyo katika hafla ya mahafali ya Kidato cha nne kwa wanafunzi wanaohitimu mwaka huu, InshaAllah. Alisema kutokana na mwenendo huo wa shule ya Forest Hill, wazazi wana kila sababu ya kujipongeza kwa kuwa wamewekeza sehemu sahihi kwa elimu ya watoto wao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa The Islamic Foundation, Sheikh Ibrahim Twaha, amewakumbusha wazazi kuwa kama walivyofanya hima katika kuwatafutia watoto wao shule nzuri, basi wanapaswa kuwathamini kwa kile walichokipata upande wa maadili kutoka shuleni hapo na kukiendeleza.

Naye Mkuu wa Shule, Mwalimu Ramadhani Sekitya, amesema kwa upande wao walimu wamewajibika kwa kuwafundisha wanafunzi walichotakiwa kufundishwa, hivyo wazazi wanatakiwa kuwalinda watoto baada ya mitihani wasije wakaharibikiwa.

Wakisoma risala yao mbele ya mgeni rasmi, wanafunzi wanaohitimu wameuomba uongozi wa taasisi hiyo kuongeza nafasi za ufadhili kwa wanafunzi wanaoshindwa kuendelea kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwemo kipato duni—kwa kuwa wapo walioanza nao lakini hawajamaliza nao masomo.

Akitoa maelekezo katika neno la shukrani kuhusiana na ombi hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya shule, Muhammad Muro, amesema utaratibu wa ufadhili upo, lakini ametahadharisha kwamba si kila atakayetaka atapewa tu; ni lazima uchunguzi ufanyike kwanza.

Shule ya Sekondari ya Forest Hill, inayomilikiwa na The Islamic Foundation yenye makao makuu mkoani Morogoro, ni miongoni mwa shule bora kwa sasa kimkoa na kitaifa, huku malengo yake yakiwa ni kuwa shule bora Afrika ya Mashariki.




# MATUKIO KATIKA PICHA

NA ABDULRAHMAN OMAR

# Forest Hill yatajwa fahari ya Morogoro





Mkurugenzi Mtendaji wa The Islamic Foundation, Sheikh Ibrahim Twaha, amewakumbusha wazazi kuwa kama walivyofanya hima katika kuwatafutia watoto wao shule nzuri, basi wanapaswa kuwathamini kwa kile walichokipata upande wa maadili kutoka shuleni hapo na kukiendeleza.














SULEIMAN MAGALI

# Naibu Waziri Mkuu ataja faida uwekezaji kwenye elimu

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini, Dk Doto Biteko ametaja faida zitakazopatikana kwa nchi za Afrika kuwekeza kwenye elimu bora, ikiwamo kuwa na mifumo thabiti ya kidijitali itakayosaidia kutatua changamoto zilizopo kwenye mataifa hayo.

Dk Biteko ameitaja faida nyingine ya kuwekeza kwenye sekta hiyo ni kutatua changamoto ya ukosefu wa elimu bora maeneo ya vijijini.

Alisema hayo jana katika mkutano wa tano wa kimataifa wa ubora wa elimu ulioandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania TenMeT.

"Tukiwekeza kwenye elimu, tutatatua changamoto ya ukosefu wa elimu bora maeneo ya vijijini, hadi kufikia 2030 Afrika inahitaji walimu milioni 17 ili kuwa na elimu bora ya msingi na sekondari, ambayo ni nyenzo ya kuwapatia wanafunzi kilicho bora," alisema.

Alisema ni lazima ifike mahali nchi za Afrika ziondokane na dhana ya utegemezi wa misaada kwenye sekta ya elimu, kwani kila anayetoa msaada matamanio yake anayepatiwa akue na kujitegemea hivyo ni lazima kila nchi iongeze rasilimali fedha kwenye sekta ya elimu.

Dk Biteko alizitaka nchi za Afrika kufikia matakwa ya utekelezaji wa kuelekeza kwenye sekta ya elimu asilimia 20 ya bajeti ya nchi.

"Katika kutekeleza hili, Tanzania tumepiga hatua kwenye kutenga na kutumia rasilimali za ndani na kuwekeza zaidi kwenye sekta ya elimu.

"Tumeongeza bajeti ya Wizara ya Elimu kutoka Sh4.7 trilioni mwaka 2021 hadi Sh6.6 trilioni mwaka 2025 na hii ni kiashiria moja wapo kwamba tumeamua kuweka rasilimali nyingi kwenye elimu ya watoto wetu," alisema.

Alisema sekta ya elimu katika nchi za Afrika bado ipo nyuma hivyo kunahitajika kuwa na nguvu kuondokana na changamoto zilizopo.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Carolyne Nombo alisema Serikali inaendelea kuboresha sekta ya elimu, akisisitiza elimu inayotolewa nchini ina viwango vya kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wake, Mratibu wa Kitaifa wa TenMeT, Martha Makala alisema mkutano huo una dhamira ya kuimarisha mifumo ya uwekezaji, kukuza uhamasishaji wa rasilimali za ndani kwa elimu jumuishi na endelevu barani Afrika.

Alisema mkutano huo utatoa mbinu ya namna ya kuboresha sera za elimu na kuja na mipango ya kuhakikisha sekta ya elimu inakuwa na uwekezaji wa uhakika.



Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TenMet, Simon Nanyaro alisema hadi kufikia mwaka 2024 watoto milioni 251 duniani wapo nje ya mfumo wa elimu na miongoni mwao milioni 100 wapo nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema katika sekta ya elimu Tanzania imekuwa ikipiga hatua hasa katika kubadili mitaala ya elimu, ujenzi wa miundombinu ya kufundishia, ujenzi wa shule za sayansi na kuajiri walimu hatua ambayo inaonesha namna sekta hiyo inavyopewa kipaumbele.

Afya
Pure Drinking water
"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com






# Siri yatajwa ukuaji sekta ya fedha ya Kiislamu Oman

Tasnia ya fedha za Kiislamu nchini Oman inatarajiwa kuvuka dola bilioni 40 kati ya nusu ya pili ya 2025 na 2026, ikichochewa na mageuzi ya kisheria yanayoendelea na mahitaji makubwa ya huduma zinazokubaliana na Shariah, kwa mujibu wa Fitch Ratings.

Taarifa iliyonukuliwa na Arab News inasema licha ya kuwa soko dogo zaidi ndani ya Baraza la Ushirikiano la Ghuba (GCC), Oman inaendelea kurekodi ukuaji wa viwango vya digiti mbili (double-digit) katika benki za Kiislamu na utoaji wa sukuk.

Kiwango cha tasnia kilikadiriwa kufikia dola bilioni 36 mwishoni mwa Agosti 2025; mali za benki za Kiislamu zikichangia takribani theluthi mbili.

Fitch inaeleza kuwa kasi hii inatokana na maboresho ya bidhaa na huduma za benki, upanuzi wa matawi na mifumo ya kidijitali, uelewa mpana wa umma, na kuongezeka kwa matumizi ya sukuk kama chombo kikuu cha ufadhili.

Mwishoni mwa Julai, mali za benki za Kiislamu zilikuwa karibu dola bilioni 23.6—ongezeko la 16.8% mwaka kwa mwaka—na sasa akaunti za Kiislamu (benki kamili na "windows") zinashikilia takriban 20% ya mali zote za mfumo wa benki.

Soko la sukuk linachangia karibu 30% ya mali zote za fedha za Kiislamu; huku deni la sukuk la Oman lililosalia lilifikia dola bilioni 7.25 katikati ya 2025, lote likiwa na tathmini ya 'BB+' na mtazamo chanya.

## Taasisi ndogo za kifedha Pakistan kufuata mfumo wa Kiislamu

**Sekta ya microfinance nchini Pakistan—ikiwemo benki na taasisi ndogo za fedha—inaendelea kubadili shughuli zake kutoka mifumo ya riba kwenda mfumo kamili wa Kiislamu kulingana na matakwa ya katiba.**

**Mwenyekiti wa Pakistan Microfinance Network (PMN) na Mkurugenzi Mtendaji wa HBL Microfinance Bank, Muhammad Amir Khan walithibitisha mabadiliko hayo katika mkutano na wanahabari uliotangulia Mkutano wa 9 wa Microfinance.**

**Taasisi kadhaa tayari zimeanzisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya sharia na nyingine ziko kwenye mchakato wa mabadiliko kamili. Ili kuhakikisha ulinganifu, taasisi zote zinawaajiri wanazuoni na wataalam wa Shariah kusimamia ufuataji na kubuni bidhaa kama murabaha, ijara na musharaka. Sekta pia imejiwekea lengo la kuwafikia wateja milioni 40 nchini kote, ikiwapa kipaumbele wanawake, wakazi wa vijijini na wakulima.**

**Mpango wa Uwezeshaji wa Kifedha unaoungwa mkono na Benki ya Dunia unalenga kuboresha ukwasi na huduma kwa wateja katika taasisi hizo, ukisaidia sekta kukabiliana na changamoto kama uharibifu uliosababishwa na mafuriko.**

**Ajenda ya mkutano ujao (7–9 Oktoba 2025, Karachi) itajikita kwenye kilimo na fedha za vijijini, ujumuishaji wa wanawake, uhimilivu wa tabianchi, ukuaji wa biashara ndogo na za kati, ushirikiano na teknolojia na bima jumuishi—ikionyesha dhamira ya kugeuza taasisi hizo ndogo za fedha kuwa kichocheo cha haki ya kijamii na maendeleo endelevu.**

## Ghana yashirikisha viongozi wa dini uanzishwaji benki za Kiislamu

**Benki Kuu ya Ghana (BoG) imefanya mashauriano na viongozi wa Kikristo na Kiislamu mapema wiki hii ili kukamilisha mfumo shirikishi wa Benki na Fedha Zisizo na Riba. Lengo ni kukamilisha kanuni mwisho wa 2025 na kuruhusu taasisi zilizopewa leseni kuanza kutoa bidhaa kuanzia 2026. Mashauriano hayo, yaliyoongozwa na Prof. John Gatsi kwa niaba ya Gavana Dkt. Johnson Asiama, yalijadili kuoanisha viwango vya kimataifa, kusimika miundo ya usimamizi wa Shariah, na kuruhusu "madirisha" ya Kiislamu ndani ya benki za kawaida sambamba na benki kamili za Kiislamu. Pia yaligusia uratibu na wadhibiti wengine ili kuwezesha masoko ya sukuk na bima ya takaful.**

**Dkt. Richmond Atuahene ametoa mapendekezo kumi ya kuwezesha u yakiwemo: maboresho ya sheria, kujenga uwezo wa wataalamu, kampeni za uelimishaji wa umma, ushirikiano mpana wa wadau wa dini zote, utawala bora, miongozo ya wazi ya Shariah, na kuimarisha mahakama kushughulikia migogoro ya mikataba isiyo na riba.**

## Milioni 53 walitembelea Misikiti Miwili Mitukufu mfungo sita

**Zaidi ya waumini na mahujaji 53,572,983 wametembelea Msikiti Mtukufu wa Makkah na Msikiti wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) Madina katika mwezi wa Rabi' al-Awwal 1447 AH, kwa mujibu wa Mamlaka Kuu ya Huduma za Misikiti Miwili Mitukufu.**

**Katika Msikiti wa Makka, waliorekodiwa kuswali ni 17,560,004, akiwemo 91,753 waliopata nafasi ya kuswali katika Hijr Ismail (Al-Hatim). Idadi ya waliotekeleza 'Umrah ilifika 12,146,516 ndani ya kipindi hicho.**

**Wakati huohuo, Msikiti wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) Madinah ulipokea 20,701,560 waumini; kati ya hao, 1,002,049 waliswali katika Al-Rawdah Al-Sharifah, na 2,071,101 walitoa salamu kwa Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) na Maswahaba wake wawili.**

**Mamlaka imeeleza kuwa ufuatiliaji wa wingi wa waumini unategemea teknolojia ya kisasa, ikiwemo vichunguzi vya vihisi vilivyowekwa katika milango mikuu ya misikiti.**

NA MWANDISHI WETU



# Mkakati wa Bandari ya Dar kushughulikia ongezeko la mizigo

**Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), ikishirikiana na waendeshaji binafsi, imetangaza hatua za kimkakati zinazolenga kuongeza ufanisi, kupunguza muda wa meli kusubiri na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha usafirishaji wa mizigo kwa eneo lote.**

Miongoni mwa miradi mikuu ni kuanzishwa kwa mfumo wa muda maalumu wa kutia nanga kwa meli katika gati namba 8 hadi 11, unaosimamiwa na Kampuni ya Tanzania East Africa Gateway Terminal. Mfumo huu, ulioanzishwa mwaka huu, unarahisisha upangaji wa ratiba za meli, kupunguza ukosefu wa uhakika wa nyakati za kuwasili na kupunguza msongamano.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Bw. Plasduce Mbossa, aliambia gazeti la The Citizen jana kuwa mbinu hiyo mpya tayari imeanza kuzaa matunda.

"Hatua hii inarahisisha upangaji na uratibu wa ratiba za meli, na kupunguza kwa kiasi kikubwa msongamano bandarini. Meli zinajua kwa uhakika ni lini zitafika gati na usahihi huu unabadilisha kabisa uendeshaji," alisema.

Mabadiliko haya yanakuja katika kipindi ambacho Bandari ya Dar es Salaam imeweka rekodi ya kipekee. Bandari hiyo ilimaliza mwaka wa fedha 2024/25 ikiwa na shehena ya mizigo ya tani milioni 27.7—ongezeko la asilimia 15 kutoka tani milioni 23.69 za mwaka uliopita na rekodi kubwa zaidi katika historia yake.

Kiwango hiki pia ni ongezeko kubwa kutoka tani milioni 18 zilizoshughulikiwa mwaka 2021/22. Kwa mujibu wa TPA, ongezeko hili linaonyesha maboresho ya miundombinu, mageuzi ya kiutendaji na kasi ya huduma zilizovutia kampuni zaidi za meli na wamiliki wa mizigo.

Katika magati namba 0 hadi 7, yanayosimamiwa na kampuni kubwa ya kimataifa ya usafirishaji DP World, uwezo umeongezwa zaidi kwa ununuzi wa kreni mbili mpya za kupakia na kupakua meli, na kufanya idadi kuwa tano. Uwekezaji huu unatarajiwa kuongeza kasi ya kushughulikia makontena na kupunguza muda wa meli kukaa bandarini, hivyo kurahisisha mtiririko wa bidhaa katika msimu wa kilele.

Uunganishaji na maeneo ya bara bado ni kipaumbele. TPA inashirikiana kwa karibu na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuimarisha njia za kuelekea Kwala Dry Port. Vichwa viwili vya treni vilivyokarabatiwa vinatarajiwa kuanza kazi kufikia Oktoba, na kuongeza uwezo wa reli kusafirisha makontena kutoka katikati ya jiji lenye msongamano.

Ujenzi wa Kituo cha Usafirishaji cha Kurasini, kituo muhimu cha kusaidia shughuli, pia unaendelea. Mradi huu sasa umefikia asilimia 40 ya utekelezaji na utatoa eneo maalumu la kushughulikia mizigo na kupunguza msongamano katika maghala ya bandari. Bw. Mbossa alisema maboresho haya yatafaidisha zaidi ikiwa wamiliki wa mizigo na mawakala wa forodha pia watatimiza wajibu wao.

NA MWANDISHI WETU

# Sababu Nicolas Sarkozy kufungwa jela miaka mitano

**Rais huyo wa zamani wa Ufaransa mwenye miaka 70 alishtakiwa kwa kufanya makubaliano na Gaddafi mwaka 2005, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ili kupata ufadhili wa kampeni yake kwa kubadilishana na kumuunga mkono Gaddafi katika jukwaa la kimataifa, wakati Libya ilikuwa ikitengwa na mataifa mengine.**

Rais wa zamani wa Ufaransa, Nicolas Sarkozy (70), amehukumiwa kifungo cha miaka mitano jela baada ya kupatikana na hatia ya ufadhili haramu wa kampeni za urais mwaka 2007, kwa kutumia fedha kutoka serikali ya aliyekuwa kiongozi wa Libya, Muammar Gaddafi.

Hukumu hiyo ya hatia inamaanisha kuwa Sarkozy, aliyeongoza Ufaransa kati ya mwaka 2007 na 2012 na alistaafu siasa rasmi mwaka 2017, atalazimika kutumikia kifungo hicho hata kama atakata rufaa.

Sarkozy alishtakiwa kwa kufanya makubaliano na Gaddafi mwaka 2005, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ili kupata ufadhili wa kampeni yake kwa kubadilishana na kumuunga mkono Gaddafi katika jukwaa la kimataifa, wakati Libya ilikuwa ikitengwa na mataifa mengine.

Rais huyo wa zamani amekana mashtaka yote na kudai kuwa kesi hiyo ina msukumo wa kisiasa.

Sarkozy tayari ametangaza kuwa atakata rufaa dhidi ya hukumu hiyo, aliyoielezea kama nzito mno kwa utawala wa sheria.

Akizungumza baada ya kusikiliza hukumu hiyo jana alidai kesi hiyo ina msukumo wa kisiasa, huku upande wa waendesha mashtaka ukidai Sarkozy aliahidi kumsaidia Gaddafi kurekebisha sifa yake mbaya mbele ya mataifa ya magharibi kama malipo ya msaada huo wa kifedha.

Katika unafuu mdogo kwake, Mahakama ya Jinai ya Paris iliagiza kuwa, Sarkozy asiwekwe rumande kwanza na waendesha mashtaka wamepewa muda wa mwezi mmoja kumjulisha lini ataanza kutumikia kifungo chake.

Jaji Nathalie Gavarino alisema kuwa, Sarkozy amehukumiwa kwa sababu aliruhusu wasaidizi wake wa karibu kutafuta msaada wa kifedha kutoka utawala wa Libya.

Wasaidizi wawili wa karibu wa Sarkozy alipokuwa rais, mawaziri wa zamani Claude Guéant na Brice Hortefeux pia walipatikana na hatia ya kushiriki katika njama ya jinai, lakini wakasamehewa katika mashtaka mengine.

Eric Woerth, aliyekuwa mweka hazina wa kampeni ya Sarkozy mwaka 2007, aliachiliwa huru.

Jaji Nathalie Gavarino alisema Sarkozy, akiwa waziri na kiongozi wa chama wakati huo, aliwaruhusu washirika wake wa karibu na wafuasi wa kisiasa aliokuwa na mamlaka nao kuwasiliana na maofisa wa Libya kwa niaba yake ili kupata au kujaribu kupata msaada wa kifedha.

Hata hivyo, Mahakama haikukubaliana na hitimisho la waendesha mashtaka kwamba Sarkozy alinufaika moja kwa moja na ufadhili huo haramu wa kampeni.

Kesi hiyo ilianza mwaka 2011, baada ya Shirika la Habari la Libya na Gaddafi mwenyewe kudai kuwa serikali ya Libya ilitoa mamilioni ya euro kwa siri kufadhili kampeni ya Sarkozy mwaka 2007.

Mwaka 2012, jarida la uchunguzi la Ufaransa Mediapart lilichapisha kile kilichodai kuwa, ni kumbukumbu ya kijasusi ya Libya ikielezea makubaliano ya ufadhili wa Euro 50 milioni.

Sarkozy alikanusha nyaraka hiyo na kuwashtaki kwa kashfa.



**Rais wa Ufaransa, Nicolas Sarkozy akisalimiana na kiongozi wa Libya, Muammar Gaddafi walipokutana Paris, Ufaransa Desemba 2007.**

ربيع ثان



Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Ukatili kwa wanafunzi ni dalili ya tatizo kubwa shuleni

Juma lililopita, vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini viliripoti tukio la mwalimu wa Shule ya Sekondari Makumbusho iliyopo Kinondoni jijini Dar es Salaam, Felix Msila kumuadhibu kikatili mwanafunzi wa kidato cha pili aitwae Khatib Salim. Kadhia hiyo ilitokea Alhamisi ya Septemba 18, 2025, na baadae picha mjongeo za tukio zilisambaa katika makundi mbalimbali ya WhatsApp.

Awali ya yote, tunaupongeza uongozi wa Shule ya Sekondari Makumbusho kwa kumfukuza kazi mwalimu huyo, pia tunaunga mkono azma ya Halmashauri ya Kinondoni ya kuchukua hatua zaidi dhidi ya mwalimu huyo.

Kama ambavyo wadau mbalimbali wamelaani na kukemea kitendo hicho, tunakubaliana nao kuwa kumuadhibu mwanafunzi kupitiliza si tu kunamletea maumivu ya kimwili bali humuathiri kisaikolojia na kumfanya awe na hofu badala ya kumfundisha.

Kwa wale waliosomea taaluma ya ualimu vyuoni wamefundishwa kuhusu saikolojia ya ujana na namna ya kuwalea vijana katika kipindi cha kubalehe, ambacho wengi wao huwa wakaidi na wasumbufu. Kwa hiyo, ni wazi mwalimu anayeijua vizuri kazi yake hawezi kumuadhibu mwanafunzi wake kikatili eti kwa sababu ya kosa moja tu alilofanya.

## Sheria inasemaje?

Kanuni ya 3 (1) ya adhabu ya viboko inasema: "Adhabu ya viboko itatolewa iwapo patatokea utovu mkubwa wa nidhamu au kosa kubwa litakalofanywa ndani au nje ya shule ambalo litaishushia shule heshima."

Kanuni ya adhabu ya viboko GN namba 294 ya Julai 31, 2002 iliyozaa Waraka wa Elimu namba 24 wa mwaka 2002 inataka adhabu ya viboko itolewe kwa kuzingatia ukubwa wa kosa, umri, jinsia na afya ya mtoto, na isizidi viboko vinne kwa tukio lolote. Aidha, sheria na kanuni hizo vinataka adhabu itolewe na mwalimu mkuu au mwalimu mwingine atakayeteuliwa na mwalimu mkuu kwa maandishi.

Kimsingi, kilichotokea Shule ya Sekondari Makumbusho na pia matukio mengine ya ukatili wa vipigo kwa wanafunzi yaliyowahi kufanyika katika shule nyingine, yanaonesha kuwa bado kuna mgogoro mkubwa wa uhusiano kati ya wanafunzi, walimu na wazazi.

Tunasema, kutoa adhabu ni njia mojawapo ya kupambana na maadili mabaya katika jamii, na ni jambo kongwe la enzi na enzi lililoelezwa katika vitabu vyote vya dini kuanzia Taurati, Zaburi, Injili na hatimaye Qur'an Tukufu.

Katika Biblia, ambayo chimbuko lake ni mafundisho ya Injili ya Nabii Isa (amani ya Mwenyezi Mungu imshuke) tunakuta andiko hili: "Usimnyime mtoto wako mapigo maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa. Utampiga kwa fimbo na kuokoa nafsi yake na kuzimu." [Taz: 'Kitabu cha Mithali: 13–14'].

Katika Uislamu, adhabu ya viboko imetajwa kama njia ya kuwaadabisha watenda maovu ya uzinifu, n.k. Mwenyezi Mungu anasema: "Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanaume wachapeni mijeledi mia moja kila mmoja wao..." [Qur'an 24:2]. Kwa upande wa watoto, Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema za Allah na amani imshukie) amesema: "Waamrisheni watoto kusali wakifikisha miaka saba na wachapeni viboko (wakiacha au kupuuza sala) wakiwa na miaka 10." [Ahmad na Abu Daudi].

Kwa hiyo, suala la watoto kuchapwa viboko, kwa mujibu wa mafundisho ya dini zote za mbinguni halina mjadala. Kinachoangaliwa ni kiasi cha hivyo viboko ambacho katika Uislamu kimeelezwa kuwa ni kipigo kisichoacha alama mwilini.

Ni jambo linalowezekana kabisa kwa walimu kurekebisha tabia za wanafunzi bila kutumia adhabu kandamizi na mwanafunzi akabadilika. Inasikitisha kuona wanafunzi wanaacha shule kwa sababu ya kukimbia viboko huku wengine wakiachwa na majeraha makubwa, ulemavu na hata vifo kwa sababu ya adhabu ya viboko.

Sasa ili kudhibiti matukio ya vipigo kwa wanafunzi ambayo kwa kiasi kikubwa huwaathiri kimwili na kisaikolojia, ni muhimu kwa mamlaka husika kuhakikisha zinawachukulia hatua stahiki walimu wote watakaobainika kuwafanyia vitendo vya ukatili wanafunzi ili iwe fundisho kwa wengine.

Mwisho, tunashauri walimu watumie mbinu mpya mbadala za malezi, zikiwamo kumpa mwanafunzi zawadi za kushtukiza (surprise), au kitu anachokipenda, au kujenga urafiki naye. Kwa mfano, mwalimu anaweza kumwambia mwanafunzi: "Ukifanikiwa kuacha tabia fulani nitakufanyia jambo fulani."

Mambo hayo tuliyoyataja yatamfanya mwanafunzi afurahie shule na kufikiria kwa kina juu ya yale ambayo mwalimu wake anataka afanye.




MAHMOUD NYAMGUMA



# Mataifa kuitambua Palestina, mwanzo wa matumaini?

Ikiwa ni juma la pili la Mkutano Mkuu wa 80 wa Umoja wa Mataifa (UNGA80) mjini New York, viongozi wa dunia wakiendelea kutoa hotuba, tunatafakari yanayozikumba jamii za Kiislamu: Gaza, Lebanon, Syria, Yemen hadi Sudan—ambako raia wanakabiliwa na hofu, ukosefu wa usalama, njaa, umasikini na milipuko ya maradhi. Je, mjadala wa UNGA80 unagusa matatizo haya ya kila siku?

Mojawapo ya matukio makubwa ni kutambuliwa kwa Taifa la Palestina. Utambuzi rasmi na mataifa 157—yakiwemo Ufaransa, Uingereza, Australia na Kanada—unaibua swali: ni mwanga wa uhuru kamili au ni shere ya muda mfupi kwa Waislamu?

Wachambuzi wanaona hii ni hatua muhimu ya kihistoria inayoongeza shinikizo la kidiplomasia dhidi ya Israel, ambayo imekaidi sheria za kimataifa kwa miaka mingi. Umoja wa Mataifa unasema zaidi ya nusu ya wanachama wake sasa wanaitambua Palestina—ishara ya mwamko wa dunia kuunga mkono haki ya Wapalestina kuwa na taifa huru.

Mataifa haya yameweka wazi lengo la kufufua suluhu ya mataifa mawili ili kuleta amani ya kudumu Mashariki ya Kati. Waziri Mkuu wa Uingereza, Keir Starmer, amenukuliwa: "Hatuwezi kuruhusu matumaini ya suluhu ya mataifa mawili kufa. Tunataka kuona Israel salama sambamba na Palestina inayojitegemea."

Kauli hii imepokewa kwa shauku na Waislamu waliochoshwa na ubaguzi, ukandamizaji na uvamizi wa ardhi ya Palestina.

Kwa mujibu wa Amnesty International, zaidi ya Wapalestina milioni 5.2 wanaishi Gaza na Ukingo wa Magharibi chini ya mashinikizo ya kijeshi na vikwazo vya Israel, huku takribani walowezi 700,000 wa Kiyahudi wakiishi katika makazi ndani ya maeneo ya Palestina kinyume cha sheria za kimataifa. Kwa hivyo, utambuzi wa mataifa 157 unaonekana kama upinzani wa vitendo dhidi ya sera hizo.

Hata hivyo, Israel inaendelea kuapa kutoruhusu kuundwa kwa taifa la Palestina. Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu alinukuliwa akisema: "Hakutakuwa na taifa la Palestina magharibi mwa Mto Jordan."

Kauli hii inakosolewa na wachambuzi wa siasa za Kiarabu kama kinyume cha haki za binadamu na sheria za kimataifa, huku Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) ikionyesha wasiwasi kuhusu ukiukwaji unaoendelea.

Wachambuzi wa Kiislamu wanaona utambuzi mpana huu kama mwanzo wa safari ya uhuru—ushindi wa kiitikadi na kisiasa unaothibitisha kuwa mapambano ya Wapalestina hayakuwa bure. Kidiplomasia, hauleti uhuru papo hapo, lakini ni chachu ya haki.

Historia ya ukombozi barani Afrika inaonyesha: mara nyingi utambuzi wa kimataifa hutangulia uhuru. Vivyo hivyo, kutambuliwa na zaidi ya mataifa 150 kunaweza kuwa msingi wa ukombozi na suluhu ya kudumu—wakati Umma wa Kiislamu ukiendelea na mshikamano wa kidugu na wa imani.

NA MWANDISHI WETU

# Trump awa mbogo UN, Palestina mpya njiani



Rais Donald Trump akihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, mjini New York.

Wakati Rais Donald Trump akisema kutambua taifa la Palestina ni "zawadi kwa Hamas," viongozi wengine, akiwamo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, wameunga mkono kuanzishwa kwa taifa huru la Palestina.

Viongozi hao wametoa maoni yao wakati wakihutubia kwa nyakati tofauti mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York, huku Rais wa Indonesia, Prabowo Subianto, akihutubia kwa mara ya kwanza mkutano huo tangu aingie madarakani. Alinukuliwa akisema:

"Nguvu haiwezi kuwa haki, haki ni lazima ibaki kuwa haki. Hakuna nchi moja inayoweza kuinyanyasa familia yote ya binadamu. Huenda kila mmoja wetu ni dhaifu peke yake, lakini hisia za ukandamizaji na dhuluma zitatufanya tuungane na kuwa nguvu itakayoshinda dhuluma hii."

Mbali na Subianto, viongozi wengine waliohutubia mkutano, wakiwamo Luiz Inácio Lula da Silva wa Brazil, Recep Tayyip Erdoğan wa Uturuki, na Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, walizungumzia umuhimu wa kuanzishwa taifa huru la Palestina.

Nchi nyingi za Ulaya, zikiwamo Uingereza na Ufaransa, zilitangaza kutambua taifa huru la Palestina. Pia, ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, zipo nchi 11, na nyingine zaidi ya 150 ndani ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambazo zimetambua taifa la Palestina.

Hatua hiyo haijamtisha Trump, ambaye kwenye hotuba yake alisema hana muda wa kusikiliza kinachoelezwa na mataifa hayo, lakini akiendelea kushinikiza Hamas kuwaachia mateka waliobaki wa Israel. Trump katika hotuba yake alisema nguvu za dunia zinapaswa kuhakikisha mateka wa Israel walioko Gaza wanarejeshwa.

"Kama ilivyo kuwahimiza kuendelea kwa mzozo, baadhi ya watu katika taasisi hii wanatafuta kutambua taifa la Palestina peke yao. Zawadi hizo zitakuwa kubwa kwa magaidi wa Hamas kutokana na uharibifu wao," alisema Trump.

Kauli ya Trump ilikuwa majibu ya moja kwa moja kwa uamuzi wa nchi kadhaa za Ulaya kutangaza kutambua taifa la Palestina. Kutambua taifa la Palestina, Trump alisema, "itakuwa zawadi kwa matendo haya ya kikatili, yakiwamo ya Oktoba 7, 2024."

Trump alipendekeza njia mbadala ya kidiplomasia:

"Badala ya kukubali madai ya fidia ya Hamas, wale wanaotaka amani wanapaswa kuungana na ujumbe mmoja: Waachilieni mateka sasa, waachilieni tu mateka. "Tunalazimika kusitisha vita huko Gaza mara moja. Tunalazimika kuvimaliza... Tunalazimika kuanza mazungumzo mara moja. Lazima tujadiliane kwa ajili ya amani. Tunalazimika kuwarudisha mateka."

## Alichosema Katibu Mkuu wa UN


Kauli ya Trump ilikuwa tofauti na hotuba ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, aliyesema suluhisho ni kuwa na mataifa mawili na kwamba utawala wa taifa la Wapalestina "ni haki, si zawadi."

Guterres, kwenye hotuba yake, alitaja hali ya Gaza kuwa "isiyovumilika" na kusema suluhisho la mataifa mawili ndilo "njia pekee ya kutoka kwenye jinamizi hili."

Kwa mujibu wa Guterres, japokuwa anakaribisha maamuzi ya mataifa mbalimbali ya kutambua suluhisho la mataifa mawili, pia alisisitiza kuwa "hakuna kinachoweza kuhalalisha mashambulizi ya kigaidi ya kutisha ya Oktoba 7, 2024, yaliyofanywa na Hamas au kitendo cha kuchukua mateka," aliongeza.

ربيع ثان

MAKALA MAALUM



NA SHEIKH SEIF RUGA

# Mtazamo wa Uislamu kuhusu saikolojia ya kushindwa

**Nafsi ya mwanadamu hupitia hali mbalimbali zinazotofautiana sana katika safari yake ya maisha. Wakati mwingine nafsi hujaa mwanga wa matumaini, ikichochewa na hamasa na ari ya kufanikisha mambo makubwa, na mara nyingine huzongwa na mawimbi ya huzuni, hofu na kukata tamaa, hivyo kujikuta ikishindwa kukabili mitihani na matatizo ya maisha.**
**Bila shaka, kushindwa kisaikolojia ni hatari zaidi kuliko kushindwa vita. Kushindwa kisaikolojia ni aina ya ukoloni wa akili na moyo, tofauti na ukoloni wa kunyonya rasilimali za dunia. Japokuwa ukoloni wa kijeshi ni mkali na unaumiza, lakini mwishowe huondoka mapema au baadaye. Kutawaliwa kisaikolojia hupenya ndani ya nafsi bila kuonekana, na kumuathiri mtu bila kufahamu hatari yake. Allah Mtukufu aliwaonya Waislamu dhidi ya hali hii ya kushindwa kisaikolojia aliposema: "Wala msikate tamaa, wala msihuzunike hali ya kuwa nyinyi mko juu, ikiwa nyinyi ni Waumini." [Qur'an, 3:139]. Hii ni dalili ya wazi kuwa imani ya kweli ni kinga ya mwanadamu dhidi ya kushindwa na kukata tamaa.**

## Madhara ya kushindwa kisaikolojia

Miongoni mwa madhara makubwa ya kushindwa kisaikolojia kwa mtu binafsi, jamii au umma, ni kunyongeka mbele ya matatizo na mitihani ya kimaisha, na kuhisi kuwa hakuna tena faida ya kujitahidi au kufanya marekebisho. Mtu hapaswi kuvunjika moyo na kuwa mnyonge katika shida inayomkabili, bali anatakiwa kujiamini na kutafuta suluhisho.

Kushindwa kisaikolojia huua matumaini ya kufanya marekebisho na kujijenga upya. Mtu au jamii inapokata tamaa kabisa, huacha kutenda, kujenga na kusahihisha mambo yaliyoharibika – na hapo ndipo anguko la kweli huanzia.

Ipo haja kwa mtu mmoja mmoja, jamii na taifa kujilinda dhidi ya maradhi haya ya kisaikolojia kwa kuimarisha imani, matumaini na azma ya kusonga mbele bila kukata tamaa. Hatupaswi kamwe kuridhia kushindwa na kukubali unyonge.

## Sababu za kushindwa kisaikolojia

Maradhi ya kushindwa kisaikolojia hayaji ghafla, ni matokeo ya mchanganyiko wa sababu za kiroho, kijamii na kiutamaduni, kama tutakavyoona katika mjadala huu.

**Sababu ya kwanza** ni udhaifu wa imani na kupenda starehe na anasa za kidunia (kujirusha kupitiliza). Madhambi humuweka mtu mbali na ulinzi wa Allah na humfanya awe mateka wa shetani. Allah Mtukufu anasema: "Na mwenye kupuuza ukumbusho wangu, basi atakuwa na maisha ya dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa ni kipofu." [Qur'an, 20:124].

**Pili,** udhaifu wa yakini kwa Allah. Siku zote ushindi hupatikana kwa wale walio na yakini ya ahadi ya Allah. Anayeshuku ahadi ya Allah au kudhani kuwa hatashinda na wala hatainuka tena hufeli kisaikolojia na anaweza hata kujiunga na makundi ya wapotevu.

**Tatu,** kutoridhia qadar (maamuzi) ya Allah. Baadhi ya watu humwabudu Allah pindi mambo yanapowaendea vizuri au wanapokuwa na maisha ya furaha na utulivu. Lakini wakipatwa na shida au mtihani mdogo tu hubadilika na kuiacha dini. Allah anasema kuhusu watu hawa: "Na miongoni mwa watu wapo wanaomwabudu Allah kwa mashaka. Akipata mema huwa na utulivu kwayo, na akipata mtihani hugeuka, basi (mtu huyu) amepata hasara duniani na Akhera..." [Qur'an, 22:11].

**Nne,** kujitenga na dini, ambayo ndiyo chanzo cha utukufu kwa Waislamu. Watu wengi hawafahamu dini yao, wanafanya ibada kwa mazoea, na wameifanya elimu ya imani kuwa nadharia badala ya kuwa mtindo wa maisha ya kila siku.

**Tano,** kuenea kwa dhuluma na kukosa msaada. Katika maeneo mbalimbali duniani Waislamu hukumbana na mateso na madhila kadha wa kadha huku wakiwa hawana wa kuwatetea. Hali hii huwachosha na kuwafanya waone hakuna matumaini hivyo kujihisi kuwa ni wadhaifu, wenye huzuni, majonzi, na waliopoteza matumaini ya mustakabali bora wa maisha yao.

**Sita,** matarajio makubwa yasiyolingana na uhalisia. Kuwa na matarajio makubwa yasiyoendana na hali halisi huchangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kisaikolojia pale mtu anapokumbwa na changamoto katika kufikia malengo yake. Mtu anayefikiri kupata mafanikio ni rahisi kama vile kuchuma maua hukata tamaa haraka pindi anapokumbwa na mtihani mdogo tu.

**Saba,** kudharau mafanikio. Mtu ambaye nafsi yake imejaa woga wa kushindwa, anapokosea hujiona duni, dhalili, mwenye hatia, na asiye na thamani wala kustahiki tena kuishi duniani.

**Nane,** kushirikiana na waliokata tamaa. Mazingira yanayomzunguka mtu huathiri sana hali yake ya ndani. Kuishi na watu waliokata tamaa, au wenye tabia ya kutamka maneno ya kuvunja moyo kama vile "Hakuna faida yoyote, huwezi kubadilisha kitu" huondoa hamasa na shauku ya kufanikiwa hata kama ulikuwa na ari ya mafanikio.

Waliofanikiwa katika nyanja mbalimbali siyo kwamba wana akili nyingi kuwazidi wengine, la hasha! Kilichofanya wafanikiwe ni shauku ya kutaka mafanikio, ubunifu, maarifa wanayowekeza kila siku, na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu wakafika hapo walipo.




# NASAHA ZA WIKI



NA YUSUFU AMINI
0787 503 085

# Tuelewe hakuna dharura ya kuishi katika haramu

Ni jambo la kufurahisha kuona huduma za bima na kibenki zinazofuata misingi na kanuni za Kiislamu zimeongezeka nchini katika kipindi cha zaidi ya muongo mmoja sasa. Benki za Kiislamu hutumia mali kama msingi wa kufanyia biashara, hazilipishi au kutoza riba, na haziwekezi kwenye biashara ya haramu kama pombe na kamari.

Hii ni katika juhudi za kuepuka kujiingiza katika mifumo ya utoaji huduma kwa njia za dhuluma kwani kwa miaka mingi Waislamu wengi hususani wa Tanzania wamekuwa wakifanya kazi na benki pamoja na kampuni mbalimbali zinazotoa huduma za kijamii kwa misingi haramu ya riba.

Kuanzishwa kwa taasisi hizi za Kiislamu ni hatua muhimu katika kuwakinga Waislamu wasiziendee huduma muhimu za kijamii na kiuchumi ambazo zinakwenda kinyume na maamrisho ya Uislamu. Mwenyezi Mungu anasema: "Enyi mliyoamini! Mcheni Allah, na acheni riba zilizobakia, ikiwa nyinyi ni waumini." [Qur'an, 2:278].

Kisha Mungu akasema tena: "Enyi mliyoamini! Msile riba mkizidisha juu kwa juu, na mcheni Allah ili mpate kufanikiwa. Na uogopeni Moto ambao umeandaliwa kwa ajili ya makafiri. Na mtiini Allah na Mtume ili mpate kurehemewa." [Qur'an, 3:130-132].

Aya hizi zinatoa hoja za ujumla kuwa Uislamu ni mfumo kamili wa maisha, na kamwe Uislamu siyo dini ya imani ya kiroho tu. Kwa hali hiyo, vipengele vyote vya maisha ya mwanadamu lazima viendane na misingi ya Uislamu, ikiwamo makatazo ya kutoza au kupokea riba na kuepuka chumo la pata potea (gharar).

Licha ya kutambua kuwa Uislamu umeweka bayana mambo yote haramu na halali, bado maadui wa Uislamu wamekuwa wakibuni taswira chanya katika kuhalalisha huduma na bidhaa za haramu. Miongoni mwa mifano hai ni kama ile ya wazinifu kuitwa wapenzi, kumbi za kufanyia maasi kupewa jina la kumbi za starehe, walevi wa pombe kuitwa wanywaji, kamari kuitwa bahati nasibu na riba kubadilishwa jina na kuitwa faida.

Licha ya hayo yote, bado Waislamu wengi wanaendelea kushikilia misimamo ya kuparamia kadhia hizi kwa hoja zisizo na maana, ikiwemo kubuniwa fursa ya kile kinachoitwa 'Kufunguliwa dunia'. Uhuru huu usiojali mipaka ya dini umekuwa kichocheo kikubwa kwa baadhi yetu kutimiza malengo ya kidunia huku tukidhani kuwa ndio ustaarabu, usasa na kwenda na wakati.

Mwenyezi Mungu anatuonya kwa kusema: "Na aminini niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha mliyonayo, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala msiuze ishara zangu kwa thamani ndogo. Na niogopeni Mimi tu, wala msichanganye kweli na uongo na mkaificha kweli hali ya kuwa mnajua." [Qur'an, 2:41–42].

Kwa hakika tumeshuhudia athari nyingi mbaya katika nchi za Magharibi ambazo kuna idadi kubwa ya Waislamu waliohamia huko wakiendesha maisha yao. Waislamu wanaoishi katika nchi hizo ni wazi kuwa wanakosa uhuru wa kutekeleza masharti ya dini yao vile inavyotakiwa. Hii ni sawa na mtu kujidhulumu nafsi yake.

Ni vema tukaelekea kule kilipo qibla kila tunapotaka kuendesha harakati zetu za kimaisha, kwani hakuna shaka kwamba kuikumbatia dhuluma ni sawa na kulikimbia jivu huku tukisahau kama tunaelekea kutumbukia kwenye moto.

Tukumbuke kila hatua na maamuzi tunayofanya yanapaswa kuegemezwa kwenye Uislamu kwa kuwa Uislamu ndiyo awali ya yote. Si busara hata kidogo Muislamu kuacha kutekeleza mambo ya msingi kwa ajili ya maslahi yake ya dunia na Akhera.

Abu Abdullahi An–Nu'uman Ibn Bashiyr (Allah amridhie) ameeleza kuwa, Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake) amesema: "Hakika halali iko wazi na haramu iko wazi, na kati ya mawili hayo kuna mambo yenye kutatanisha ambayo wengi hawayajui. Basi atakayejiepusha na mambo yenye kutatanisha, kwa hakika amejitakasia dini yake na heshima yake; na atakayejiingiza kwenye mambo yenye kutatanisha atakuwa ameingia katika haramu..." [Bukhari na Muslim].

Kwa kuzingatia hadith hiyo, tukae tukijua kuwa katika dunia ya sasa hakuna dharura ya kukumbatia mambo ya haramu. Tukumbuke Siku ya Kiyama tutasimama mbele ya Mola wetu Muumba na atatuhukumu kwa uadilifu juu ya yale tuliyoyatenda. Hivyo, ili tuweze kufuzu siku hiyo tunawajibika kusimama imara katika kukabiliana na mitihani ya ulimwengu.



UKHTI FATIMA SS

# Elimu ni zaidi ya asomacho mtoto darasani



**Wazazi wengi hufikiri kwamba elimu ni mchakato unaoanzia rasmi mtoto anapoingia darasani. Hata hivyo, tafiti na uzoefu wa maisha ya kila siku vinaonesha kuwa elimu ni pana zaidi kuliko vitabu na madawati.**

**Mtoto huanza kujifunza mara tu anapofumbua macho yake duniani; na kwa hakika, asilimia kubwa ya ukuaji wa ubongo hutokea ndani ya miaka mitano ya mwanzo ya maisha. Hivyo, kila tukio na kila mazingira anayokutana nayo mtoto hujenga msingi wa maisha yake ya baadaye.**

**Wanasayansi wanasema kuwa karibu asilimia 90 ya ukuaji wa ubongo hutokea kabla ya mtoto hajafikisha miaka mitano. Katika kipindi hiki, mtoto hujifunza lugha, hisia, tabia na uelewa wa kijamii. Hii ina maana kuwa hata kabla ya kuanza shule rasmi, watoto tayari wanaunda misingi ya uelewa na ustadi watakaoutumia darasani. Kusoma vitabu na wazazi, kutambulishwa herufi, namba na nyimbo ni mwanzo wa safari ya kielimu.**

## Kujifunza nje ya darasa

Elimu si lazima iwe ndani ya kuta nne za darasa. Shughuli kama michezo ya pamoja, kushiriki katika kazi ndogo ndogo za nyumbani, au kutembelea maeneo ya kijamii (kama masoko, mashamba au maktaba) hujenga stadi muhimu za maisha.

Kwa mfano, mtoto anaposhirikishwa kupika, hutambua vipimo, maumbo na hata kufanya mahesabu ya msingi. Michezo ya ubunifu hujenga uwezo wa kufikiri kwa kina na kutatua matatizo.

## Kujifunza kupitia jamii na mazingira

Mtoto anaposhirikiana na familia na jamii, anajifunza maadili, heshima, mshikamano na utu. Uislamu unasisitiza kuwa malezi bora yanaanza nyumbani, ambapo wazazi wanapaswa kuwa walimu wa kwanza kwa watoto wao.

Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) alisema: "Kila mtoto huzaliwa katika fitra, ni wazazi wake humfanya Myahudi, Mkristo au Mpagani." [Bukhari na Muslim]. Kauli hii inatufundisha kwamba malezi na elimu ya awali ndiyo yanayounda mwelekeo wa mtoto.

## Umuhimu wa maandalizi ya shule

Tafiti zimeonesha kuwa watoto wanaoingia shule wakiwa tayari kielimu na kijamii huwa na nafasi kubwa ya kufanikiwa. Nchini Marekani, utafiti ulionesha zaidi ya asilimia 40 ya watoto walipoanza shule ya awali hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa kusoma.

Hali hii inapelekea tofauti kubwa ya ufaulu darasani. Hata kwetu Tanzania, changamoto ya maandalizi ya shule ipo. Watoto wengi vijijini hawapati fursa za kujifunza nyumbani, jambo linalowaathiri wanapoanza shule.

## Umuhimu wa mazingira salama na yenye upendo

Elimu si tu kuhusu herufi na namba, bali pia kujenga uwezo wa kiakili, kihisia na kijamii. Mtoto anapokua kwenye mazingira yenye vurugu, dhuluma au msongo wa mawazo, maendeleo yake huathirika.

Kinyume chake, mtoto anayekua kwenye nyumba yenye upendo, nidhamu na utulivu huwa na uwezo bora wa kujifunza na kuwasiliana.

Uwekezaji katika elimu ya awali huokoa gharama za muda mrefu. Wataalamu wanasema kuwa kwa kila shilingi moja inayowekezwa kwenye elimu bora ya awali, jamii huokoa shilingi 11 zinazoweza kutumika baadaye kwenye masuala ya uhalifu, afya au elimu. Hii ni dalili kuwa maandalizi ya mapema huzaa matunda makubwa.

## Jukumu la jamii na wazazi

Wazazi wanapaswa kutambua kuwa elimu inaanzia nyumbani. Kusoma vitabu na watoto, kuzungumza nao, kuwashirikisha kwenye kazi ndogo ndogo na kuwapeleka maktaba au misikitini ni sehemu ya mchakato wa kujenga akili na tabia zao.

Vilevile, jamii nzima ina jukumu la kuwekeza kwenye vituo vya malezi na elimu ya awali vinavyohimiza maadili mema na ujuzi wa maisha.

# ALI BIN ABI TWALIB: Khalifa wa nne wa Mtume

## Kifo chake

**Kifo cha Swahaba huyu mtukufu kilitokea mikononi mwa dhalimu aliyejulikana kwa jina la Abdurrahman bin Muljim. Wataalamu wa historia wanasimulia kuwa Muljim pamoja na Burk bin Abdillah na Amr bin Bakr Attaymiy na wengine watatu miongoni mwa Makhawarij, walikutana Makka katika msimu wa hija kujadiliana kuhusu hali ya Waislamu na viongozi wao. Katika kikao hicho, watu hao waliwataja kwa maneno mabaya viongozi wakuu wa dola ya Kiislamu, hususan Ali, Muawiya na Amr bin Al-As (Allah awaridhie). Walieleza huzuni juu ya ndugu zao waliouawa katika vita vya Nahrawan, kisha wakaulizana: "Sasa tufanye nini? Kwa nini tusiwauwe hawa viongozi wapotofu na kuipumzisha jamii ya Waislamu na balaa yao?"**

**Ndipo bin Muljim akasema: "Mimi niachieni Ali." Burk akasema: "Mimi nitamuua Muawiya." Na Amr bin Bakr akasema: "Mimi nitatosha kumuua Amr bin Al-As." Ikawa ni mpango hatari uliokusudiwa kutekelezwa usiku wa tarehe 17 Ramadhan, mwaka wa 40 Hijriya.**




### Utekelezaji wa mpango wa mauaji

Baada ya makubaliano, kila mmoja alielekea eneo la tukio. Bin Muljim akaenda Kufa makao ya Ali (Allah amridhie), Burk akaenda Sham makao ya Muawiya, na Amr bin Bakr akaelekea Misri makao ya Amr bin Al-As.

Usiku wa tukio, Amiril-Muuminina Ali (Allah amridhie) alitoka kuelekea msikitini akitangaza: "Swala, enyi watu, swala." Ghafla alitokeza Abdurrahman bin Muljim akampiga kwa upanga utosini, akisema: "Hukumu ni ya Allah, si yako wewe Ali na wenzako."

Ali (Allah amridhie) akaanguka huku damu zikimtoka usoni na zikamchafua ndevu zake.

Ali akabebwa nyumbani kwake, na bin Muljim akakamatwa na kuletwa mbele yake. Ali akasema: "Nafsi kwa nafsi. Nikifa kwa shambulizi hili, naye muueni; nikipona nitaamua mwenyewe nini la kufanya."

### Wasia wa Ali kwa wanawe

Hali ya Amiril-Muuminina ilivyozidi kudhoofika, alimuusia wanawe Hasan na Husein (Allah awaridhie) kumcha Allah, kushikamana na swala na zaka, kuzuia hasira, kuunga udugu, kuwa wapole kwa wajinga, kuendelea kujifunza dini, kuchunguza habari kabla ya kutoa maamuzi, kudumu kusoma Qur'an, kufanya wema kwa majirani, kuamrisha mema na kukataza maovu, na kujiepusha na maasi.

Aidha, aliwausia kumfanyia wema ndugu yao wa baba mmoja, Muhammad bin al-Hanafiyya, na yeye pia akawausia awaheshimu kaka zake. [Taz. Rijaal wanisaa hawla Rasoul, uk. 174–175].

Baada ya wasia huo, Ali (Allah amridhie) aliaga kwa maneno: "Nakuachieni kwa Allah na nawatarajia rehema na amani." Kisha hakutamka neno lolote ila: "Laa ilaaha illa Allah," mpaka alipokata roho.

### Hatima ya waliopanga mauaji

Ama Burk, alipojaribu kumuua Muawiya (Allah amridhie), hakuweza kufanikisha jaribio lake. Alimjeruhi tu, kisha akakamatwa na kuuawa. Muawiya akatibiwa na kupona.

Amr bin Bakr naye alikusudia kumuua Amr bin Al-As (Allah amridhie), lakini usiku huo Amr hakutoka msikitini kwa kuwa alikuwa mgonjwa. Badala yake alimtuma Kharija bin Hudhafa. Amr bin Bakr akamdhania ndiye Amr bin Al-As, akamuua. Baadaye akakamatwa na kupelekwa mbele ya Amr bin Al-As, na akaamrishwa auawe.

Hivyo ndivyo jaribio la kumuua Muawiya na Amr bin Al-As lilivyoshindikana, na ndivyo ulivyofungwa ukurasa wa uhai wa mtu muadilifu, mchamungu, mwenye ikhlasi, jasiri, muaminifu wa Imani na itikadi, ndugu na mkwe wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie), baba wa Hasan na Husein (Allah awaridhie), Khalifa wa nne wa Mtume: Ali bin Abi Twalib bin Abdil-Mutwalib (Allah amridhie).

Tunamuomba Allah amfunike kwa msamaha na radhi Zake. Ameen.




AFYA YAKO

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Utafiti: Unywaji mdogo wa maji huongeza homoni ya msongo wa mawazo

**Maji ni uhai. Ndiyo sehemu kubwa ya miili yetu na msingi wa mchakato mingi ya kibaiolojia. Hata hivyo, utafiti mpya uliochapishwa katika Journal of Applied Physiology umeonyesha kwamba watu wanaokunywa maji kidogo kila siku huwa na ongezeko kubwa la homoni ya msongo wa mawazo (cortisol) wanapokumbana na hali za kiakili zinazowatia wasiwasi.**
**Hii inafafanua kwa nini ukosefu wa unywaji bora wa maji umehusishwa na hatari ya maradhi ya muda mrefu.**

## Jinsi ukosefu wa maji unavyoathiri mwili

Mwili unapokuwa katika hali ya ukosefu wa maji, dalili hutokea wazi: mkojo unakuwa mweusi na mchache, kinywa hukauka, na mtu hukosa nguvu.

Lakini utafiti huu unaonesha athari nyingine iliyo hatari zaidi – msisimko wa cortisol unaopita kiasi. Cortisol hufuata mzunguko wa saa wa mwili, lakini pale inapoongezeka kupita kiasi, huathiri kinga ya mwili, mfumo wa metaboli, na hata kuongeza uvimbe.

Kwa muda mrefu, hali hii inaweza kuongeza hatari ya maradhi ya moyo, figo, na kisukari. Watafiti walibaini kuwa watu wanaokunywa chini ya lita 1.2 kwa siku mara nyingi huwa na viwango vya juu zaidi vya cortisol kuliko wale wanaofuata ulaji wa maji unaopendekezwa.

## Kuhusu utafiti uliofanyika

Utafiti ulihusisha washiriki wenye afya njema, wasio na magonjwa ya usingizi, moyo, au metaboli, wenye umri wa kati ya miaka 18–35. Waligawanywa katika makundi mawili: wale wanaokunywa maji kidogo (LOW) na wale wanaokunywa maji mengi (HIGH). Kila kundi lilikuwa na washiriki 16.

Kwa siku saba, walirekodi kiwango cha vinywaji walivyotumia. Baadaye wakafanyiwa jaribio maarufu la kisaikolojia (Trier Social Stress Test), kisha sampuli za mate na mkojo zikachukuliwa kupima viwango vya cortisol na viashiria vya unywaji maji.

Matokeo yalionesha kuwa kundi la LOW lilikuwa na viwango vya juu zaidi vya cortisol kabla na baada ya jaribio. Ingawa viwango vya wasiwasi vilikuwa karibu sawa kati ya makundi yote mawili, wale waliokunywa maji kidogo walionesha mwitikio mkubwa zaidi wa mwili kwa msongo wa mawazo.

## Maana ya matokeo kwa afya yetu

Tafiti hizi zinaonyesha kuwa unywaji wa maji si suala la kiu pekee, bali pia linahusiana moja kwa moja na ustawi wa akili na mwili. Kuongezeka kwa homoni ya msongo huongeza uwezekano wa matatizo ya kiafya, hasa yanapodumu kwa muda mrefu.

Kwa Tanzania, ambako joto na shughuli za mwili ni za juu, upungufu wa maji unaweza kuwa tatizo kubwa zaidi. Watu wengi hutumia soda, juisi zenye sukari, au kahawa badala ya maji safi. Lakini vinywaji hivi haviwezi kuchukua nafasi ya maji kama chanzo cha msingi cha unyevu mwilini.

## Mifano halisi ya maisha yetu

Tuchukulie mfano wa dereva wa bodaboda anayetumia masaa mengi barabarani bila maji ya kutosha. Msongo wa mawazo unaotokana na barabara zenye foleni, pamoja na joto, unaweza kumfanya mwili wake kuzalisha cortisol nyingi zaidi. Kadri anavyoendelea na tabia ya kunywa maji kidogo, ndivyo anavyoweka afya yake kwenye hatari ya shinikizo la damu au magonjwa ya figo.

Aidha, kwa wanafunzi na wafanyakazi wa ofisi, ukosefu wa maji unaweza kupunguza uwezo wa kukabiliana na mitihani au vikao vya kazi vinavyohitaji umakini mkubwa. Mwili unapotulia kwa maji ya kutosha, akili pia hupata utulivu.

Mtazamo wa Kiislamu

Uislamu unatufundisha kuthamini afya zetu. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alisema: "Hakika mwili wako una haki juu yako." (Bukhari). Kunywa maji ya kutosha ni sehemu ya kutunza mwili huu tuliopewa kama amana.

Zaidi ya hapo, Qur'an inataja maji mara nyingi kama neema kubwa ya Mwenyezi Mungu: "Na tumeteremsha kutoka mbinguni maji yenye baraka..." (Qur'an 50:9). Maji siyo tu yanatulisha mimea bali pia yanaweka mwili katika mizani.

Kwa hiyo, kunywa maji ni kitendo cha kiafya na pia cha kiroho – ni njia ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema alizotupa.

Utafiti mpya unatuonesha wazi kuwa kunywa maji kidogo kila siku si tatizo dogo. Ni chanzo cha ongezeko la homoni ya msongo wa mawazo, hali inayoweza kuathiri afya zetu kwa muda mrefu. Kwa Watanzania, hasa katika mazingira yenye joto na shughuli nyingi, ujumbe ni wazi: tuzidishe maji safi, tupunguze vinywaji vyenye sukari, na tuone afya zetu zikiboreka.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, kulinda mwili kwa kunywa maji ni sehemu ya ibada na shukurani. Afya bora huimarisha ibada na maisha ya kila siku. Hivyo basi, kila glasi ya maji tunayoinywa ni hatua ya kulinda mwili na roho zetu.




## MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Huyu ndiye kiongozi tumtakaye

Amir wa Waumini, Umar bin Khattwab (Allah amridhie) aliwaomba watu wa Hims (Syria) wamwandikie majina ya masikini wote ili awagawie mali kutoka hazina ya Waislamu (Baytul–Maal). Majina yalipomfikia alishangaa kuona jina la Swahaba Mtukufu, Sa'id bin Amir Al–Jumahi (Allah amridhie), ambaye alikuwa Gavana wa Hims likiwa miongoni mwa majina ya watu masikini!

Umar akawauliza watu wa Hims: "Inawezekanaje Gavana wenu awe miongoni mwa watu masikini?" Wakamjibu: "Yeye hutumia mshahara wake wote kuwasaidia masikini na wenye mahitaji, na husema: 'Nifanyeje wakati nimeteuliwa kuwajibika kwao mbele ya Allah Mtukufu?"

Umar aliposikia hivyo akalia sana huku akisema: "Sifa njema anastahiki Allah Ta'ala, ambaye amejaalia miongoni mwa viongozi wangu mtu mwenye hali kama hii." ***[Taz: 'At–Tabaqat al–Kubra', juz. 4, uk. 269; Mukhtasar Tarikh Dimashq; na Al–Haythami: Majma' al–Zawaid, mlango wa fadhila za masikini]."***

### Mafundisho ya tukio

Uongozi ni dhamana ambayo watu wengi huishindania pasina kujua uzito wake. Wengi miongoni mwetu hutumia dhamana ya uongozi kwa maslahi binafsi wakifuja mali za umma, na wengine hutumia vyeo vyao kufanya ufisadi katika ardhi. Dhuluma, uonevu, kiburi na ubabe ndiyo sifa zinazowalinda viongozi wengi wa zama hizi, huku wakitumia mamlaka yao kwa njia mbaya na kufanya maisha ya watu yaharibike kutokana na maamuzi yao.

Tukio hili linatupa taswira ya kiongozi anayejali maslahi ya raia, shida, taabu na matatizo yao. Gavana Sa'id bin Amir (Allah amridhie) aliuishi uhalisia wa watu wake kiasi cha kufanana nao katika hali zao. Haikushangaza kuona jina la Sa'id katika orodha ya watu masikini kwa sababu maisha yake ndiyo yalikuwa maisha ya watu aliyowaongoza na kuwasimamia.

### Uongozi ni kuwajibika, si fursa ya kujinufaisha

Katika Uislamu, uongozi ni kuwatumikia watu na si fursa ya kujinufaisha. Kutokana na huruma na uchungu aliokuwa nao kwa raia wake, Sa'id bin Amir (Allah amridhie) alikuwa akitumia kiasi kikubwa cha mali zake kusaidia watu wa mji wake hadi akawa masikini. Kwa kifupi, Sa'id alikuwa muwajibikaji hodari kwa masikini.

Huu ni mfano wa huruma ya kweli inayotakiwa kwa viongozi. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Asiyeonesha huruma kwa watu, Allah hatomhurumia." [Bukhari na Muslim].

### Viongozi kuchanganyika na raia

Viongozi wengi wa zama hizi wanaishi maisha tofauti na raia wa kawaida, wanatumia rasilimali za nchi kwa maslahi yao kwanza, na hawana hisia za machungu wanayokumbana nayo watu kwa kuwa wao na familia zao wanaishi vizuri, tofauti kabisa na maisha ya watu wengine.

Sa'id bin Amir alikuwa mtu wa kawaida sana, hakutafuta umaarufu wala kuishi maisha ya anasa, na alikuwa mnyenyekevu hata aliposhika nafasi ya juu ya uongozi. Juu ya hilo, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Hakuna yeyote anayenyenyekea kwa ajili ya Allah isipokuwa Allah humnyanyua." [Muslim].

Mara kwa mara Sa'id alijitolea kwa hali na mali na kwa ukarimu kutatua changamoto za watu wake. Viongozi wa namna hii wanajua fika kuwa umasikini si aibu, ni hali wanayopitia watu wengi na inahitaji ufumbuzi kutoka kwa viongozi wanaojali hali za watu.

### Mfano wa kiongozi bora

Katika tukio hili tumeshuhudia Amir wa Waumini, Umar bin Khattwab (Allah amridhie) akiomba orodha ya majina ya masikini wanaoishi Hims (Syria) ili awagawie mali kutoka hazina ya Waislamu (Baytul–Maal). Huu ni mfano wa viongozi tunaotakiwa kuwa nao katika dunia ya sasa.

Umar hakusubiri kuletewa malalamiko bali alikuwa akifuatilia kwa karibu hali za watu masikini katika miji mbalimbali na kuhakikisha wanasaidiwa. Pia alisikiliza malalamiko ya watu dhidi ya viongozi aliyowapa mamlaka katika sehemu mbalimbali na kuwafuatilia

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari






JUNAYNAT ALLY DAMA

# Namna ya kufundisha watoto kumtegemea Allah



**Katika malezi ya Kiislamu, jukumu kubwa la mzazi si tu kuhakikisha mtoto anakua kimwili na kielimu, bali pia kumjenga awe na moyo wa kumtegemea Allah (subhanahu wa ta'ala) katika kila jambo. Hali hii inaitwa tawakkul — kutambua mipaka ya uwezo wetu na kuamini kwamba msaada wa kweli unatoka kwa Mola Muumba.**

## Msingi wa fitra ya mtoto

Kila mtoto huzaliwa akiwa na fitra safi ya kumtambua Mola wake. Wazazi wanapomlea katika mazingira ya kumkumbusha Allah, fitra hii hubaki hai katika msimamo sahihi.

Hivyo, kazi ya mzazi si kuingiza kitu kipya, bali ni kuendeleza kile ambacho tayari kimewekwa na Allah ndani ya mtoto. Hii inahitaji mawasiliano ya karibu, mazungumzo yenye upendo, na mfano wa vitendo.

## Mosi: Kuwa mfano wa tawakkul

Watoto hujifunza zaidi kwa kuona kuliko kusikia. Wazazi wanapokumbana na changamoto na bado wakaonesha subira na kumtegemea Allah, watoto hujenga imani hiyo mioyoni mwao na kuiga mfano huo katika nyakati zao ngumu.

Qur'an inatufundisha: "Na anayetawakali na Mwenyezi Mungu, basi Yeye humtosha" [Qur'an, 65:3]. Tukiamua kuishi kwa mfano huu, watoto watajua kwamba nguvu na suluhu ya maisha yote ipo kwa Allah Aliyetukuka.

## Pili: Kueneza upendo wa ibada mapema

Mtoto mdogo hapaswi kushurutishwa ibada kwa hofu, bali kuoneshwa uzuri na mapenzi yaliyo ndani yake. Kusali pamoja kwa furaha, kumsomea Qur'an kwa sauti tamu, na kumfundisha dua za kila siku humjengea mtoto hisia chanya ya kumtegemea Allah.

Ikiwa chini ya miaka minane, si muda wa kumkaripia kwa kutoshiriki, bali wa kumvutia kupitia upendo na rehema. Baada ya umri huo anaweza kuchapwa kwa kadri ya umri wake.

## Tatu: Hadithi na simulizi za wema

Hadithi za Mitume na Maswahaba ni hazina kubwa. Kumhadithia mtoto namna Nabii Ibrahim (amani ya Allah imshukie) alivyomtegemea Allah aliporushwa kwenye moto, au namna Nabii Musa (amani ya Allah imshukie) alivyovuka bahari akitegemea msaada wa Mola, humfundisha kwamba matatizo makubwa hayana nguvu mbele ya Allah.

Simulizi hizi zikitolewa kwa lugha rahisi na zenye msisimko humjengea mtoto heshima na imani thabiti kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.

## Nne: Kumfundisha kuchukua hatua na kumwachia Allah matokeo

Tawakkul si uvivu. Tawakkal ni kufanya jitihada kisha kuamini matokeo yako mikononi mwa Allah. Wazazi wanapaswa kumfundisha mtoto kujaribu, kuwa na subira na kurudia tena jambo analolitafuta bila kukata tamaa.

Msingi ni kumweleza kwamba juhudi zake hazipotei, kwani Allah anaziona na kuzithamini na atamlipa kwa nia yake njema na juhudi aliyoiweka katika jambo la kheri. Hii humjengea moyo wa kustahimili changamoto za maisha.

## Tano: Kuunganisha changamoto na subira

Watoto wanapokumbana na matatizo, kama kushindwa mtihani au kugombana na rafiki, wazazi wawaongoze kuona kuwa changamoto ni sehemu ya mpango wa Allah na wasichukulie kuwa Allah amewatelekeza.

Qur'an inatufundisha: "Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaomtegemea" [Qur'an, 3:159]. Hivyo, kila jaribu lina nafasi ya kumkuza kiimani na kiakili, na kumfanya ajifunze kusubiri na kushukuru kwa kikubwa na kidogo alichopata.

## Sita: Kujenga nyumba yenye upendo na utulivu

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alisema: "Ikiwa Mwenyezi Mungu atataka kheri kwa familia, huingiza upole katika nyumba yao" [Musnad Ahmad].

Hii ina maana nyumba yenye heshima, utulivu na huruma humfanya mtoto ajisikie salama na kuamini kwamba kumtegemea Allah ni njia ya kupata amani. Hii ndiyo msingi wa afya ya akili na ustawi wa kiroho.

UKHTI FATIMA SS

# Namna ya kuondoa mawazo mabaya akilini

**Kila binadamu hukutana na mawazo hasi katika safari ya maisha. Mawazo haya yanaweza kuibuka ghafla, kujirudia mara nyingi na kugeuka kuwa mzigo mzito wa kisaikolojia. Wataalamu wa afya ya akili wanasema hali hii ya negative spiraling au kuzungukwa na mawazo mabaya, huweza kuharibu furaha, kuleta msongo wa mawazo na hata kupunguza ari ya kufanya mambo ya msingi ya kila siku.**

**Lakini jambo la kutia moyo ni kwamba, kwa mbinu sahihi za kisaikolojia, kijamii na kiroho, tunaweza kuyadhibiti mawazo haya kabla hayajatawala maisha yetu.**

## Kwa nini tunanaswa na mawazo mabaya?

Wanasayansi wa saikolojia wamegundua kuwa ubongo wa binadamu una "upendeleo wa kiasili" wa kuzingatia zaidi mambo mabaya kuliko mazuri (negativity bias). Hii ilikuwa kinga kwa mababu zetu waliolazimika kuwa macho dhidi ya hatari, lakini leo inasababisha mtu kuishi na wasiwasi usio wa lazima.

Vichocheo vikuu vilivyotajwa mara nyingi katika tafiti mbalimbali ni matukio yenye msongo kama migogoro ya kifamilia, matatizo ya kifedha au migongano kazini.

Vichocheo vingine ni upweke na kujitenga kunakopelekea mtu kushindwa kupata faraja kutoka kwa wengine, mitandao ya kijamii na kulinganisha maisha na ya wengine, kukosa usingizi na afya duni ya mwili, pamoja na historia ya majeraha ya kihisia (trauma) ambayo hufanya mawazo hasi kujirudia mara kwa mara.

## Mbinu za kudhibiti mawazo mabaya

Mosi, njia muhimu ni kutumia mindfulness (yaani kuwa hadhiri) na mbinu za kutuliza akili. Hii inamaanisha kujifunza kuishi katika sasa. Kupumua kwa makini, kuangalia mazingira au kuhisi hisia za mwili ni mbinu rahisi zinazosaidia kukata mzunguko wa mawazo.

Pili, mtu anatakiwa kupinga mawazo hasi kwa hoja. Wataalamu wanashauri mbinu ya "Catch it, Check it, Change it". Kwanza unayakamata mawazo mabaya, kisha unayauliza maswali ya kimantiki: je, kuna ushahidi kweli? Je, ningeambia rafiki yangu jambo hili? Hatimaye, unayabadilisha kwa mawazo yenye mizani zaidi.

Tatu, uandishi na kujadili na nafsi ni kinga kubwa. Kuandika mawazo kwenye daftari husaidia kuyaona kwa uwazi na kuyaweka katika muktadha. Hii hufanya kazi sawa na kushiriki hisia au kuongea na rafiki wa karibu.

Nne, ni muhimu kutafuta msaada wa kijamii. Kuzungumza na mtu unayemwamini huleta unafuu mkubwa. Mtazamo wa nje, ambao wewe upeo wako wa akili haukufikia kuuona, mara nyingi huondoa taswira mbaya inayojengwa na akili.

Tano, mtu anaweza kujinusuru kwa shughuli chanya na kubadili mazingira. Mazoezi ya mwili, kusikiliza muziki wa kutuliza, kushughulika na shauku binafsi au hata matembezi mafupi huondoa akili kutoka kwenye duara la mawazo hasi. Aidha, kubadili mazingira kama kutoka ndani kwenda hewani ni mbinu ya pattern interruption inayozuia mawazo mabaya kuendelea.

Sita, kufanya kubadili mtazamo (reframing) au ni silaha kubwa. Badala ya kuona tatizo kama mwisho wa safari, ulione kama fursa ya kujifunza. Mbinu hii ya kiakili huitwa cognitive reframing na imethibitishwa kupunguza msongo wa mawazo.

Saba, mtu anapaswa kuishi kwa ratiba na kuifuata kwa nidhamu. Ratiba ya kila siku huleta uthabiti wa kiakili. Kujua nini kipo mbele hupunguza wasiwasi unaotokana na kutokuwa na uhakika wa mambo yajayo.

Nane, kuendeleza shukrani na huruma binafsi ni tiba ya ndani. Mawazo ya shukrani, kama kuandika mambo matatu ya kushukuru kila siku, hubadilisha mwelekeo wa akili. Vilevile, kujiambia maneno ya faraja na kujihurumia kunakata sauti ya lawama ya ndani.

Tisa, ni muhimu kuwa na uangalizi na udhibiti wa vichocheo. Mtu ajiulize, nini hasa hunichochea kuingia kwenye mawazo mabaya? Ikiwa ni mitandao ya kijamii, aweke mipaka. Ikiwa ni watu fulani, aweke nafasi.

Kumi, hatua ya mwisho ni msaada wa kitaalamu inapobidi. Ikiwa mawazo haya yameanza kuathiri kazi, mahusiano au kusababisha mawazo ya kujiumiza, msaada wa kitaalamu ni jambo la lazima. Tiba kama Cognitive Behavioral Therapy (CBT) imeonyesha mafanikio makubwa.

## Mtazamo wa Kiislamu

Nimalize kwa kuweka msimamo wa Uislamu, ambao unatufundisha kwamba akili na moyo hupata utulivu kwa kumkumbuka Allah. Qur'an inasema: "Bila shaka kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia." [Qur'an, 13: 28].

Aidha, Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alitufundisha dua za kujikinga na huzuni na wasiwasi. Mfano: "Ewe Mwenyezi Mungu, najikinga kwako na wasiwasi na huzuni, najikinga kwako na udhaifu na uvivu..." (Hadithi sahihi). Hii inaonesha kuwa Uislamu unakiri changamoto za kiakili na unatupa nyenzo za kuzikabili.

Kuzingatia Swala tano kwa wakati wake, kufanya dhikr, kusoma Qur'an na kushirikiana na Waislamu wema ni nyenzo za kiroho zinazosaidia kupunguza nguvu ya mawazo mabaya.

NA UKHTI FATIMA



# Wanawake wajasiriamali wa mfano katika Uislamu

**Biashara na ujasiriamali ni sehemu muhimu ya maisha ya kijamii na kiuchumi. Katika historia ya Kiislamu, wanawake walionesha uwezo mkubwa katika nyanja hizi kwa kuzingatia maadili na mipaka ya dini.**

**Mfano bora na wa kwanza kabisa ni Bi Khadija bint Khuwaylid (Allah amridhie), mke wa kwanza wa Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie).**

## Kisa cha Bi Khadija

Bi Khadija alizaliwa katika familia yenye heshima kubwa ya kikabila na kibiashara katika Quraysh. Baada ya kifo cha baba yake, alirithi biashara kubwa na yenye changamoto. Hata hivyo, katika mazingira ya kijamii yaliyotawaliwa na wanaume, aliweza kuendesha biashara kwa uadilifu, hekima na ujasiri.

Aliwasafirisha bidhaa kwenda Sham (Syria) na Yemen kupitia misafara mikubwa. Umahiri wake ulimpatia majina ya heshima kama Ameerat Quraysh (Malkia wa Quraysh) na al-Tahira (Mchamungu).

Khadija hakuwahi kupoteza heshima yake kama mwanamke Muislamu. Alijulikana kwa uadilifu wake katika biashara na hakuwahi kufanya jambo kinyume na misingi ya Kiislamu.

Ni katika msingi huu alipomchagua Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) kusimamia misafara yake, akivutiwa na uaminifu na uadilifu wake. Hatimaye, walifunga ndoa na Bi Khadija akawa sio tu mfanyabiashara mashuhuri, bali pia nguzo ya kwanza ya kuunga mkono risala ya Uislamu.

## Mifano ya wanawake wengine katika historia

Mbali na Khadija, historia ya Kiislamu imejaa mifano ya wanawake waliothibitisha uwezo wao katika biashara na kazi za mikono. Asma bint Abu Bakr (Allah amridhie) alikuwa jasiri na mwenye bidii, akilima shamba na kubeba mazao kwa mikono yake.

Zainab bint Jahash (Allah amridhie) alijulikana kwa ushonaji na kazi za ngozi, mapato yake akiyatumia kwa sadaka. Mke wa Abdullah ibn Mas'ud (Allah amridhie) alitengeneza bidhaa za mikono kwa ajili ya matumizi ya familia, jambo lililosifiwa na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie).

Al-Shifa bint Mu'awwiz (Allah amridhie) alikuwa kiongozi wa soko la Madina, ishara ya heshima kwa nafasi ya wanawake katika biashara.

Aidha, Sauda bint Zam'a (Allah amridhie) alijipatia riziki kupitia uchakataji wa ngozi, huku wanawake wengine kama Khaula na Thaqafia (Allah awaridhie) walijihusisha na biashara ya manukato. Hawa wote walichangia kwa bidii zao bila kuacha ibada na majukumu ya kifamilia.

## Masharti na maadili ya kiislamu katika ujasiriamali

Uislamu unaruhusu mwanamke kumiliki mali, kufanya biashara na kusimamia shughuli zake mwenyewe. Lakini ujasiriamali wa Kiislamu unaongozwa na masharti na maadili maalum. Kwanza, mwanamke anatakiwa kuheshimu mavazi na haya ya Kiislamu, akihakikisha biashara haimvui heshima yake mbele ya watu.

Pili, anatakiwa kutoacha majukumu ya kifamilia na malezi ya watoto kwa sababu ya biashara; jukumu la mama bado linabaki la msingi. Tatu, biashara zote lazima ziwe ndani ya mipaka ya halali; ni haramu kujihusisha na ribaa, bidhaa zilizokatazwa au udanganyifu.

Nne, mwanamke anatakiwa kudumisha uaminifu na uadilifu katika mikataba, bei na ubora wa bidhaa zake, kwani hii ndiyo siri ya mafanikio ya Bi Khadija na wajasiriamali wengine na tano, nia kuu ya biashara inapaswa kuwa kutafuta radhi za Allah na si kujiongezea sifa au mali pekee.

Kwa kuzingatia masharti haya, ujasiriamali wa Kiislamu hauwi tu kazi ya kiuchumi bali ibada inayompeleka muumini karibu zaidi na Mola wake. Hii ndiyo sababu wanawake wa mwanzo katika Uislamu waliweza kufanikisha biashara kubwa huku wakibaki wachamungu na watiifu.

## Mafunzo kwa wanawake wa leo

Wanawake wa Kiislamu wa sasa wanaweza kujifunza kutoka historia hii kwamba ujasiriamali haumaanishi kupoteza nafasi zao za kifamilia au kiimani.

Bali ni fursa ya kujipatia riziki halali, kusaidia jamii na kueneza maadili ya Kiislamu. Mafanikio ya kweli yanapatikana pale ambapo biashara inafanywa kwa misingi ya uadilifu, uchaji Mungu na kujitolea.

Historia ya Kiislamu imejaa mifano ya wanawake wajasiriamali waliothibitisha kwamba mwanamke anaweza kuchangia katika jamii kupitia biashara bila kuacha wajibu wake kwa Allah na familia. Kutoka kwa Bi Khadija hadi Asma, Zainab na Al-Shifa, tunaona urithi wa wanawake wachapa kazi, wachamungu na waadilifu.